

**REPUBLIC OF KENYA**  
**COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI**

**THE HANSARD**

**Wednesday, 10<sup>th</sup> May, 2017**

*The House met at the County Assembly Chambers,  
Malindi Town, 2.30 p.m.*

*[The Speaker (Hon. Kahindi) in the Chair]*

**PRAYERS**

**COMMUNICATION FROM THE CHAIR**

EVALUATION OF ASSETS IN WARD OFFICES BY THE COUNTY ASSEMBLY SERVICE BOARD

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Hon. Members, I have two communications to make. One, it is a requirement that towards the end of this term, the County Assembly Service Board (CASB) is required to do an evaluation of assets that the County Assembly has procured in the past; that includes your ward offices for the elected Members. We are actually required as a matter of urgency to go to each and every ward office and do a stock-take of the things that the County Assembly purchased so that an inventory is made for purposes of the next Assembly.

This is a long exercise. We wanted to start it earlier but due to technicalities here and there, it has not been possible. So, I wanted to bring to your attention that beginning tomorrow for the elected Members, you will receive a phone call from the Clerk either today or tomorrow, preferably today, of the wards which the Board will be visiting. We will simply be making an appearance and taking inventory of the things that were bought then and what we still have in the offices and then further communication will come. Now, this is a requirement for handing over for the Board. So, the Board will not be cleared unless it has left an inventory with the Clerk and in this case we are talking about the Majority Leader, the Minority Leader and the Speaker.

It is part of our duty to ensure that is done. Kindly, I would like to urge you to co-operate. You do not have to be there as an MCA, we will meet whoever will be there even a watchman; we have no problem so as long as we are able to confirm that the table, the seats and an inventory of the laptops are there. There are very basic clearance procedures which need to be done before the next election. For that, I think you will be hearing from us.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

## DEMISE OF HON. ALI BAKARI, MCA SHIMO LA TEWA WARD

Number two, I want to give five minutes for Members of the County Assembly (MCAs) to eulogize our departed *mheshimiwa*. Since we put him to rest, the County Assembly has not been able to convene. I have been here since Monday and we have had no quorum but I think it is very important that we spend five minutes of our time to eulogize him for the record since his death was untimely and then the House will continue with its normal business.

**Hon. Mwambire:** Thank you very much Mr. Speaker. On behalf of the Orange Democratic Movement (ODM) of Kenya, I take this opportunity to eulogize our departed friend and a vanguard of the party. Hon. Bakari was a true friend and a defender of the party until his death. In our records, hon. Bakari had intended to resign from the party but it was a very big miracle that happened that he died before presenting the papers of resignation from the party so we still remember that Bakari was an ODM Member until his death. Hon. Bakari has been a close friend to me and even to the Leader of Majority. He was a friend to me before elections and I played a very big part in strategizing how hon. Bakari was to get that seat at Shimo la Tewa.

There were a number of voters from up-country who had been brought to Mtwapa with an intention of getting that seat but we went there, we sat and strategized. Even though I was also a contestant in Vitengeni Ward at that time, we took time to strategize and when we were elected, we became very close friends with him and even the Leader of Majority, hon. Mwingo, was his chief campaigner. Hon. Bakari used to understand the issues that we have in this House and even had very clear projections. Hon. Bakari had a heart problem and we are very thankful to the County Assembly through the CASB for the actions you took.

Hon. Bakari wanted to go to India, according to the records, for his heart treatment but miraculously the person who was to accompany the late hon. Bakari to India died even before taking him. As he was looking for another person to go with him, his mother also passed on. Now, nominations were around the corner so he wanted to spare some time to go through the nominations before going to India and accidentally some of his close friends never participated in the nominations and because of that reason, Hon. Bakari lost the nomination with less than 10 votes. Although we cannot say that hon. Bakari died because of the loss of nominations, he was very determined because he gave a very elaborate speech after the tallying, he was very strong and we knew that he was going to remain very firm and he was going to campaign for the Governor and the party although he was to contest as an independent candidate. We know there are some issues but fate normally pays tax to no man and that is why we do not have that elegant Member in our party and in this Assembly.

We will miss him but everybody has his or her own way of departing from this earth because it is a provision in all the religious books and everybody expects that at some point we will die. That is the reason why in most cases when we are making budgetary allocations we also budget some money for such eventualities Mr. Speaker. We are taking insurance knowing that at some point we will die. That was the last part of hon. Bakari. We accept that because he is the second Member in this Assembly to pass on, we came as 53 Members and I pray that we conclude this term with the remaining Members. Let me believe as we are about to conclude this term, the rest of us will live longer so that we can see the true fruits of devolution.

We are the mid-wives of devolution in this country, hon. Bakari being one. Those who will be re-elected, those who will be elected in the National Assembly or in any other capacities should remain very firm and alive so that they can guide those who will be coming so that the

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

true part which we had inspired to have as the pioneers of this Assembly can be followed to the letter. That is our expectation, so let us keep on praying, and let us believe that regardless of our political affiliations and perceptions; let us pray for each other. We do not know who will come back. We cannot laugh at any other person simply because somebody failed in the nominations or somebody is an independent candidate because we are all in a theater and we do not know who will wake up first after the operations. So let us all keep on praying that we succeed and make sure that hon. Bakari's aspirations are kept to the best of our beliefs and ability in the same spirit. Thank you very much and I take this opportunity to pray for hon. Bakari's soul to rest in eternal peace. Amen.

**Hon. Hamza:** Asante sana Bw. Spika kwa kunipatia mda huu pia mimi kuchangia moja ama mawili kuhusu kifo ambacho kimemfika mheshimiwa Bakari ambapo tunavyozungumza kwa sasa yeye amekuwa marehemu. Bw. Spika, nikichukua wakati huu kusema ukweli labda naweza kukosa maneneo ya kujieleza hasa nikiangalia kwamba Bakari alikuwa ni mcheshi, mzungumzaji mzuri wa watu, na ilikuwa ni vigumu sana kukosana na watu.

Mheshimiwa Bakari kwa ule mda mchache ambao nimemjua alikuwa si mtu wa kuficha jambo. Ni mtu ambaye anazungumza peupe na ikiwa kuna mahali ambapo umemkwaza yeye mara nyingi alikuwa akifungua moyo wake. Hivyo basic, nikizungumza namaanisha tumepoteza mtu ambaye alikuwa ni mwema sana kwetu na zaidi ya hayo, nina imani kwamba matendo yake yalimtangulia na pia ninaimani kwamba Mwenyezi Mungu ataweza kuhifadhi roho yake. Kifo cha mheshimiwa Bakari kimetupata katika hali ya sintofahamu ikiwa ni vigumu kuamini kwamba mheshimiwa Bakari alikuwa ametuacha. Mimi binafsi niliposikia kifo chake, kwanza niliona kwa mitandao sikuamini. Nilifikiri kwamba ni mazungumzo tu lakini nilichukua jukumu kwanza kwa kuhofia, nikapiga simu mtu ambaye najua ni rafiki yake wa karibu.

Nilipompigia aliniambia kuwa hana ufahamu kwa sababu hata yeye alichukua hatua ya kupiga nyumbani na ikiwa habari hiyo ya kifo haijambikwa. Bw Spika, nilichukua ujasiri na nikaamua kumpigia mheshimiwa Bakari moja kwa moja kwa sababu namba yake niko nayo. Wakati huo nilipopiga ndipo iliposhikwa na Ken Chonga na akaniambia kwamba mheshimiwa Bakari ametuacha sasa hivi. Hivyo ikanibidi nikamrudia tena yule mtu ambaye nilikuwa nimemwambia mara ya kwanza ndio akafanya ufuatili na baadaye akahakikisha kwamba yale niliyokuwa namwambia ni ya ukweli. Mheshimiwa Spika, kile cha msingi zaidi na kuweza kufahamu ni kwamba kama alivyotangulia kuzungumza Mwanachini wa Spika, ni kwamba Bakari alikuwa ni mkakamavu sana na alikuwa mwanachama thabiti katika chama cha Orange Democratic Movement (ODM). Kwa hivyo katika haya ambayo yamezungumzwa ni kwamba ODM inasikia masikitiko makubwa sana kwamba imepoteza mwanachama wake ambaye ni muhimu sana.

Pia nataka kusema kwamba ODM inafaa kukaa chini na kuona kwamba masaibu haya ya mheshimiwa Bakari yalianzia wapi. Kwa sababu kama walikuwa wanajua yeye alikuwa ni mtu muhimu, mimi ninahakika kifo chake katika hali yoyote ambayo kiko iwapo hapa tutazungumza na tuzunguke huku na huku lakini mwisho wa siku ni kwamba kifo cha Bakari kimetokea katika masaibu mengine ambayo hayawezi kuelezeka na ni kwa sababu lazima tuelezane wazi kwamba labada uchaguzi ule kuna mahali ambapo ulichangia kwa sababu mheshimiwa Bakari tayari alikuwa amenuia na sisi kama waislamu tuna imani kwamba kabla jambo lolote ulifanye ukilitilia nia huwa kuna mahali linatembea.

Maathalani mheshimiwa Bakari alikuwa ametia nia kwamba anataka kugombea kiti cha Shimo la Tewa kama mgombea huru tayari nia ile ilikuwa ishaonyesha wazi kwamba yeye

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

alikuwa na mwaswala na chama kile ambacho labda kwa sasa wanaweza kusimama na kusema kwamba alikuwa ni mtu wao muhimu, lakini Bakari alikuja akagundua umuhimu wake ulikuwa umechukuliwa kama kipande cha papa. Kwa hivyo, ukizungumzia hivyo ni kwamba mheshimiwa Bakari kadri tunavyozungumza yeye anajua ni masaiibu gani zaidi yale ambayo yalimtokezea.

Bw Spika, nataka kuzungumza na niweke wazi kwamba mheshimiwa Bakari yale ambayo yalimfika mpaka kifo chake Mungu mwenyewe ndiye anayejua lakini ninaimani kabisa kwamba hakupewa muda ule ambao unatakikana kusikizwa ama hakupewa wakati mzuri kwa yale ambayo yalitokea na kuna uwezekano kwamba kuna mambo ambayo yaliendelea kichinichini na kadri ya ule ugojwa wake aliokuwa nao hakuweza kuyahimili na kuvumilia na ikafika mahali mauti ikambeba. Kila jambo lina chanzo na sababu lakini ukweli wa mambo uzungumzwe kwamba kifo cha Bakari kikambeba. Kila jambo lina chanzo, kila jambo halikosi sababu lakini ukweli wa mambo ni uzungumzwe kwamba kifo cha Bakari kimeletwa katika hali ya mtafaruku, chama chenyewe cha ODM chajua. Asante sana Bw Spika, na ninaombea roho ya mheshimiwa Bakari mwenyezi Mungu aiweke mahala pema peponi kwa sababu sote hapa twapita. Asante, Mungu atubariki sote.

**The Leader of Majority** (Hon. Mwingo): Asante sana mheshimiwa Spika. Nataka nichukue hii nafasi na Mungu atusaidie ili tuwe wavumilivu kwa ile huzuni ambayo tuko nayo. Kama ni mtu ambaye anamjua mheshimiwa Bakari basi mimi ninamjua Bakari vilivyo. Mheshimiwa Bakari tumetoka katika lokesheni moja ya Mtwapa. Wodi hizi mbili ya Shimo la Tewa na Mtepeni ziko katika lokesheni moja ya Mtwapa. Bakari tumejuana tangu tulipochaguliwa kama Madiwani miaka mitano iliyopita. Nimekuwa na Bakari bega kwa bega. Ni mambo ya kuhuzunisha kwa sababu mimi ndiye mtu wa kwanza niliyempigia simu akiwa anaelekea Nairobi. Yeye alikuwa hawezi kufanya jambo lake la kiuongozi kukosa kunifahamisha kama kiongozi mwenzake.

Tukiangalia katika ule uchaguzi wa mchujo uliofanyika, mheshimiwa Bakari tulifanya kazi na yeye bega kwa bega, wale wafuasi wake walikuwa wafuasi wangu na tukapiga kura vizuri lakini kwa sababu ya yale yaliyotekea, yeye na kamati zake wakaamua lazima aende Nairobi ili akajiandikishe ili asimame kivyake. Ilipofika asubuhi kabla hajatoka alinipigia simu akaniambaia mheshimiwa Mwingo mimi saa hii niko kwenye basi ninaelekea, nikamjibu wewe elekea. Lakini cha kushangaza ilipofika jioni ninapata hizo habari kwenye mitandao kwamba mheshimiwa Bakari ametuacha. Sikuamini, nilichukua simu nikapiga na hiyo simu niliyopiga ilishikwa na afisa wa polisi na akanieleza mheshimiwa Bakari ametuacha.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kuhuzunisha lakini kama vile tunavyojua ni kwamba katika vitabu vya Mungu ni lazima tukubali kwa yote maana kila mmoja ameandikiwa siku zake za kuenda. Lakini kama vile mheshimiwa Hamza alivyosema, kuna mambo mengi sana ambayo yalifanyika wakati ule wa mchujo lakini mimi mwenyewe nilimwambia Bakari hayo asiyaweke kwenye moyo na kama ameamua kujiandikisha asimame kama yeye mwenyewe, afanye hivyo na mimi nitamsadia na nilikuwa nimejitolea kabisa nihakikishe kuwa ninamsaidia kivyovyote ili kiti cha Shimo la Tewa akichukue.

Hivi tunavyoongea, watu wa Shimo la Tewa bado wanajiuliza kiti kile watampatia nani. Kwa hivyo, ombi langu ni kuwasihhi waheshimiwa wenzangu tumuombe ili roho yake Mungu aiweke pahala pema peponi maana sote tunamjua vile tumeishi na yeye. Asante sana mheshimiwa Spika.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**Hon. Mlanda:** Asante sana mheshimiwa Spika kwa nafasi hii. Mimi ninataka pia nichukue nafasi hii kushirikiana na wenzangu kutoa salamu zetu za rambi rambi kwa mheshimiwa mwenzetu Bw. Bakari ambaye alituacha kwa hali ya kutatanisha sana.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli salamu hizi sote hatukuzipokea kwa njia nzuri kwa sababu afadhali mtu aumwe aweze kuacha salamu ama urithi kwa familia yake ili hata mtu ukiondoka katika ulimwengu huu ile familia iwe inajua umeongea nao kuliko umeacha familia yako na umeaga unaenda safari kuangalia mambo ambayo yatasaidia wale wananchi waliokupigia kura, Bw. Spika, kabla kufika kule unakoenda familia ipate habari ya kwamba umeaga ukiwa kwenye kiti cha gari. Salamu hizi tulizipokea kwa mshangao na kama vile wenzangu walivyotangulia kuongea kuhusu mambo ya siasa, mimi langu ni ombi kwa vyama vile husika na sisemi ni ODM peke yake lakini hali ya kunyang'anyana ushindi inaweza kuchangia madhara mengi hasa kwa sisi wanasiasa.

Mfano huu ambao umetupata kulingana na marehemu lakini hata hivyo kuna mwenzetu saa hii hajui hali yake iko vipi kwa sababu amepitwa na akanyang'anywa ule ushindi wale lakini huyo bado yuko hai na tuko naye. Lakini usiwe ni mwenendo kwa wale ambao hasa wanahusika zaidi kwa kupendelea uchaguzi. Wakati kama huo ukifika unawezajikuta umzima na ukaangushwa na *heart failure* pale pale ama ukapandwa na *pressure* kwa sababu umeonewa halafu likaja hili jina la marehemu kama vile tulivyompoteza mheshimiwa Bakari. Kwa hivyo, wale wahusika wa vyama uchaguzi ni uwe wa haki na mtu akipata haki yake ya ushindi apewe haki yake. Nazungumza haya kwa huzuni sana kwa sababu mheshimiwa Bakari kabla hajasafari tulikuwa tumeongea na akaniuliza mawaidha nikampatia.

Kama vile wenzangu walivyotangulia kusema kuwa alikuwa akiongea na waheshimiwa wenzake kuhusu ile njia ambayo angeweza kupita ili kufaulu kwa malengo yake lakini mbali na hayo, sioni kwamba kifo chake kilifikia wakati ule. Nina hakika kililetwa na majonzi na huzuni na vile vitendo ambavyo alitendewa wakati huu wa *nominations*. Tukiwa hapa kama waheshimiwa ni marafiki kiasi cha kwamba mtu anakutolea jino hapa lakini kumbe ana kuuma mgongoni, si tabia nzuri na nataka nirudie si tabia nzuri! Ikiwa mtu humpendi muonyeshe humpendi kuliko mtu umuonyeshe unampenda halafu kumbe unamuuma mgongo.

Ninazungumza hivi nikiwa naskia uchungu sana kwa sababu nimekua karibu na mheshimiwa Bakari na mimi mwenyewe pamoja na wananchi wangu wa Ganda tulichukua nafasi wakati ule tulipopata habari tukaenda kungoja mwili mpaka ukaingia. Niko na dadangu anaishi pale Mtwapa, tukaenda kukaa kwake mpaka mwili ulipokuja. Wacha nikubali kwamba binadamu huenda siku zake zikifika na nikubali kwamba mwisho wa binadamu ni mauti. Wacha nimuombe rafiki yangu, mheshimiwa mwenzangu Mungu azidi kumuhifadhi kwa njia yoyote ile kulingana na vitendo vyake kama mheshimiwa tuliyekua naye katika Bunge hili. Asante sana kwa kuniapatia wakati huu.

**Hon. Mramba:** Asante sana Bw. Spika. Nami nasimama kupeana risala za rambi rambi kwa niaba yangu mimi mwenyewe na kwa niaba ya familia yangu. Mheshimiwa Spika, tumemkosa sana mheshimiwa Bakari ambaye tulijuana hapa Bungeni na tumeheshimiana sana kiwango ambacho hakina kifani. Chama cha ODM na vile vile Bunge hili limepoteza mtu wa maana sana ambaye pengo lake litakua gumu kulijaza. Hivyo basi, ombi langu ni kwamba Bunge hili liweze pia kusaidia ile familia yake na ikiwezekana hata kama kuna kijana wake ambaye anaweza kupatiwa ajira hapa Bunge ningeomba kwa niaba yangu mimi na wenzangu aweze kupatiwa ajira angalau tuweze kumkumbuka mheshimiwa Bakari. Tunaamini kwamba kifo kinakuja wakati wowote na hivyo basi ni changamoto kwetu sisi ambao tuko hai leo kwamba ni

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

vyema utayarishe maisha yako vile unavyotaka yawe kwa sababu kifo kinakuja wakati wowote ila tu ni kwamba kinatafuta sababu. Mimi naamini kwamba siku zake Bakari zilikuwa zimefika na alikuwa ameandikiwa kwamba atakufa kwenye gari tena mbali na kwao. Hayo ni mambo yake Mwenyezi Mungu na hivyo basi ningeomba kwamba tuwe pamoja tunapokutana hapa na tuweze kuikumbuka familia yake ambayo imemkosa sana mtu wao ambaye ndiye aliyekua tegemeo kubwa. Najua kila mmoja anasikia uchungu hasa mheshimiwa Arafa ambaye amekua karibu na mheshimiwa Bakari sana. Hivyo basic, ningeomba kwa unyenyekevu kwamba kwa niaba yangu na familia yangu namuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mheshimiwa Bakari mahali pema peponi. Asante.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Hon. Mramba, you always have something interesting to say even in the middle of a crisis. I did not want to cut anybody short because this Assembly has so far lost two Members of the County Assembly and that is a tragic loss so I had to give everybody an opportunity to eulogize hon. Bakari and honestly and sincerely speaking, may his soul rest in eternal peace. Now, let us move to the next Order.

## PAPERS

### REPORT ON THE VETTING OF THE NOMINEE FOR THE POSITION OF CHAIRPERSON MBEGU FUND BOARD

**Hon. (Ms.) Zawadi:** Thank you Mr. Speaker, Sir. Today being Wednesday, 10<sup>th</sup> May, 2017, I beg to lay the following Paper on the Table; The Report of the Planning, Trade and Cooperatives Committee on the vetting of the nominee for the appointment to the position of the Chairperson Mbegu Fund Board.

*(Hon. (Ms.) Zawadi laid the Report on the Table)*

## STATEMENT

### ORDER OF BUSINESS FOR THE WEEK STARTING MONDAY, 15<sup>TH</sup> TO FRIDAY, 19<sup>TH</sup> MAY, 2017

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Hon. Pascal, please proceed.

**The Leader of Minority** (Hon. Pascal): Thank you Mr. Speaker for giving me an opportunity to read through the Order of Business for the week commencing Tuesday, 16<sup>th</sup> May, 2017:-

Tuesday 16<sup>th</sup> May, 2017 at 9:00 a.m. there will be tabling of the Report of the Budget and Appropriations Committee on the Kilifi County Budget estimates for the Financial Year 2017/2018.

On Tuesday, 16<sup>th</sup> May, 2017 at 2:30 p.m. there will be a Motion on the Adoption of the Report on the Planning, Trade and Cooperation Committee on the Vetting of the Nominee for the Appointment to the Position of the Chairperson Mbegu Fund Board.

Then there will be two Statements; one by hon. Emmanuel Chai to the County Executive Committee Member in charge of Roads and Infrastructure. The second Statement will be by hon. Naphtali Kombo to the County Executive Committee Member in charge of Agriculture, Livestock and Fisheries.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

On Wednesday at 2.30 p.m. there will be a Motion on the Adoption of the Report of the Budget and Appropriations Committee on the Kilifi County Budget Estimates for the FY 2017/2018.

Thank you Mr. Speaker, Sir.

## MOTION

### ADOPTION OF THE REPORT ON THE KILIFI COUNTY SUSTAINABLE FOREST RESOURCES MANAGEMENT POLICY, 2016

**Hon. (Ms.) Muthoka:** Thank you, Mr. Speaker, Sir. On behalf of the Chairperson and the Committee on Delegated County Legislation I beg to move:-

THAT, this House adopts the Report of the Select Committee on Delegated County Legislation on the Kilifi County Sustainable Forest Resources Management Policy, 2016 laid on the Table of this honourable Assembly on Monday, 27<sup>th</sup> February, 2017.

I call upon hon. Matano to second.

*(Hon. Matano seconded)*

*(Question proposed)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Yes hon. Matano.

**Hon. Matano:** Asante mheshimiwa Spika. Basi acha nisimame na kuunga mkono Ripoti ya Kamati ya *Delegated County Legislation*. Ni muda mrefu kidogo Ripoti hii ililetwa ndani ya Bunge hili na wakati huo haikuweza kupita kwa sababu ya mambo mawili, matatu. Kamati ilipewa tena jukumu ikaweze kurekebisha maswala yaliyokuwa na kufikia leo, sisi kama Kamati tulikaa chini tukashughulikia Ripoti ile. Tulipopata Ripoti hii tulikaa na washikadau na wakaweza kutoa maoni yao na baada ya maoni hayo kujadiliwa, ilionekana kwamba ile daftari iliyoletwa mara ya kwanza ilikuwa na matatizo na Waziri pamoja na washikadau na wanakamati watengeneza daftari ya pili.

Palipotengenezwa ile daftari ya pili, Kamati ilikuwa na jukumu ya kuangalia ni jinsi gani itaweza kuleta ile sheria ambayo inafaa. Tulipoangalia vizuri tukagundua kwamba ile daftari ya pili ndiyo inaweza kuwafaa wakaazi wetu wa Kilifi, ndiposa sisi kama Kamati tukafikia uamuzi wa kwamba tutoe Ripoti ile nyengine ambayo ililetwa na waziri mara ya kwanza ili baadaye tuweze kuidhinisha ile ya pili ambayo ilitengenezwa na waziri, washikadau na wanakamati wote. Kwa hivyo, langu ni kufahamisha Bunge hili kwamba iwapo katika Kamati yetu kuna jukumu kama hili, tuna uwezo wa kupeana maamuzi yasiyozidi moja kama vile ambavyo wakati wa nyuma maana nakumbuka mimi ndiye niliweka Ripoti hii mbele ya Bunge hili. Waheshimiwa wengi walikuwa wamesema itawezekanaje yale yaliyoibuka ni mengi lakini tumeamua tunakataa Ripoti yote? Sasa nataka kueleza Bunge kwamba Kamati hii kulingana, nataka kueleza kwa njia ya kiingereza Bw Spika, "*Statutory Act*" hiyo kidogo kwa Kiswahili imenitoka, inaturuhusu kama Kamati kuweza kufanya uamuzi wa kukataa moja na kukubali nyengine. Kwa hivyo, kama Kamati tulikataa ile iliyoletwa ili tuweze kukubali ile ambayo ilitengezwa na Kamati na wale washikadau. Asante Bw Spika.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Hon. Matano, you have only told us what transpired but you have not told us the content of the policy and whether you support it. I do not know whether I did not get you.

**Hon. Matano:** Asante sana mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza nimeanza kusema kwamba naunga mkono Ripoti hii.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Yes but for somebody who has just sat in I think it is very difficult to know what you are talking about. You have not said anything about the Report itself. You have only told the House of what transpired and the events that have been surrounding the Report but you have not gone into even a paragraph of the Report. What is the policy all about?

**Hon. Matano:** Asante mheshimiwa Spika. Sheria ambayo ilikuwa iko mbele yetu ilikuwa ni sheria ya kuhusu Misitu na Chemichemi. Ilipoletwa katika Bunge hili sisi kama Kamati tukaalika wale wataalamu ambao wako na utaalumu zaidi juu ya mambo ya chemichemi ndiposa yale maoni yao waliyoyaleta ikabidi tuweze kutoka na daftari nyengine ambayo lingewafaa watu wa Kilifi mheshimiwa Spika.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Okay thank you. Any other person? Yes hon. Pascal.

**Hon. Pascal:** Thank you Mr. Speaker, for giving me an opportunity to contribute towards the Motion on the Floor.

Mr. Speaker, I stand to support the adoption of this Motion because it dwells much on the conservation of the forest and as a County, we have seen the dwindling forest reserves and for us to contain these forests, there should be proper laws and policies that will guide the community on how we can have these important forests.

As we speak, we all understand that Kilifi is affected by forest division and we have seen a lot of charcoal burning and if that is not contained in good time, we stand to welcome a very devastating desert that is in the offing and this is the right time for us as a government to ensure that we come up with laws that will guide us and the public.

Mr. Speaker, as I went through this policy I saw that it contains a lot of proper ways that if followed then in one way or the other we will go back to the days where forest cover was large and we saw how rain was attracted and the other issues that come along with the forest cover. As we now speak, we have seen people moving up and down looking for food and we understand that food resources are normally contained when we have enough rainfall and that can be gotten when we have enough rain cover.

So Mr. Speaker, the effects of drought is what we are seeing today that as we have depleted the forest cover, we have lacked rain and it is upon us now to ensure that we put up measures that will take us bit further as far as forest conservation is concerned. I call upon the hon. Members to embrace this Report and pass it so that we can now start having proper conservation of forests and by so doing then we will be on the right track. Thank you Mr. Speaker, I call upon Members to support this Motion.

*(Question put and agreed to)*



**ADJOURNMENT**

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Hon. Members, in the absence of any other business in the Order Paper, I move to adjourn the House. Thank you very much.

**The House rose at 3.12 p.m.**